WILL of GOD
316

## Je, Nawezaje Kujua Mapenzi ya Mungu?

*"Msifuatishe tena mfano wa ulimwengu huu, bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu. Ndipo mtaweza kujaribu ili kuthibitisha mapenzi ya Mungu yaliyo mema, yanayopendeza na kamilifu machoni pake."* Warumi 12:2

Kujua na kutekeleza mapenzi ya Mungu ni muhimu sana. Kuwa kama Yesu. Alisema kwamba alikuja duniani, *"Si ili kufanya mapenzi yangu, bali mapenzi yake yeye aliyenituma,"* Yohana 6:38. Sehemu kubwa ya mapenzi ya Mungu hutumika kwa Waumini wote kwa njia ileile. Hata hivyo, Mungu ana mapenzi ya kibinafsi kwa ajili ya Waumini wote ambayo Yeye huyafunua polepole kadiri unavyoimarika katika uhusiano wako na Yeye kupitia uaminifu wa kila siku. Unaweza kujua mapenzi ya Mungu. Atakupa ufahamu. *Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote wala usizitegemee akili zako mwenyewe; katika njia zako zote mkiri yeye, naye atayanyoosha mapito yako,"* Mithali 3:5-6. Unaweza kujua mapenzi ya Mungu ya jumla kwa ajili ya Waumini wote kutoka kwenye Biblia. Unaweza kujua mapenzi Yake kwako binafsi kama machanganyiko usiokinzana wa Neno Lake na maisha yenye utiifu. Kutokana na msingi wa utiifu, unaweza kubaini na kutii mapenzi Yake kwako. Muulize Baba. Pata mwongozo kutoka kwenye Neno Lake, hekima Yake, watu Wake, na amani Yake. Unapojua mapenzi ya Mungu, mtii.

**MAPENZI YA MUNGU YA JUMLA.** Sehemu kubwa ya mapenzi ya Mungu ya jumla inapatikana kwenye amri, kanuni, na mifano ya Biblia. Biblia ndio chanzo cha msingi cha kujua mapenzi ya Mungu kwa ajili ya maisha yako. *"Neno lako ni taa ya miguu yangu na mwanga katika njia yangu,"* Zaburi 119:105.

1. Amri. Kuna amri nyingi kwenye Biblia kwa ajili ya Waumini wote kama vile, *"Furahini siku zote; ombeni bila kukoma; shukuruni kwa kila jambo, kwa maana haya ndio mapenzi ya Mungu kwa ajili yenu katika Kristo Yesu,"* 1 Wathesalonike 5:16-18. Na *"Mapenzi ya Mungu ni ... mjiepushe na uasherati,"* 1 Wathesalonike 4:3. Yesu alisema, *"Kama mnanipenda, mtazishika amri zangu,"* Yohana 14:15. Elewa muktadha wa amri husika. Mungu alimwambia Nuhu ajenge safina, Mwanzo 6:14. Mungu hajakuambia ufanye hivyo. Mungu alimwambia Daudi aende Hebroni, 2 Samweli 2:1. Mungu hajakuambia ufanye hivyo. Usiondoe amri kutoka kwenye muktadha wake.

2. Kanuni. Kuna kanuni za Kibiblia unazopaswa kufuata. Kanuni ya usimamizi mzuri iko katika Luka 16:1-13. Gharama ya kuwa mwanafunzi iko mwishoni mwa Luka 14. Kanuni ya kuwatafuta waliopotea iko katika mifano mitatu ya Luka 15. Fuata kanuni hizo na zingine zilizo katika Biblia.

3. Mifano. Amri na kanuni za Biblia zinakuonyesha mapenzi ya Mungu ya jumla kwa ajili ya maisha yako. Biblia ina mifano tunayopaswa kufuata. Mfano bora zaidi ni maisha ya Yesu. Baada ya kuosha miguu ya wanafunzi, Yesu alisema, *"Mimi nimewawekea kielelezo kwamba imewapasa kutenda kama vile nilivyowatendea ninyi,"* Yohana 13:15. Tunapaswa kufuata mfano Wake wa unyenyekevu, Wafilipi 2:3-5. Tunapaswa kufuata hatua Zake, *"Ninyi mliitwa kwa ajili ya haya, kwa sababu Kristo naye aliteswa kwa ajili yenu, akiwaachia kielelezo, ili mzifuate nyayo zake,"* 1 Petero 2:21. *"Katika hili twajua kuwa tumo ndani yake: Yeyote anayesema anakaa ndani yake hana budi kuenenda kama Yesu alivyoenenda,"* 1 Yohana 2:5-6.

**ONYO.** Mungu hasemi uwongo, Zaburi 119:160. Mungu hatakuongoza wala kukuambia usitii Neno Lake. Yesu anatupatia viongozi ili kutufunza, Waefeso 4:11-14. Hata hivyo, kuna walimu wengi wa uwongo, 2 Timotheo 4:3-4. Usiamini kamwe kwamba Mungu anakuambia usitii Neno Lake. Mungu hawezi kufanya hivyo. Ikiwa kiongozi wa kanisa atakuambua usitii Neno la Mungu, hilo ni fundisho la uwongo.

**MAPENZI YA MUNGU KWA MTU BINAFSI.** Mungu ana mapenzi kwa Waumini binafsi, Zaburi 32:8, Mithali 3:5-6. Tii mapenzi ya Mungu ya jumla. Kisha, ili kujua mapenzi Yake kwako binafsi, mwombe Mungu kwa dhati na atakuonyesha. Tafuta jibu Lake kutoka kwenye Neno Lake, hekima Yake, watu Wake, na amani Yake.

**Omba**. Omba sala ya Daudi, *"Nifundishe kufanya mapenzi yako,"* Zaburi 143:10. Mtume Paulo aliomba kwamba Waumini wa Kolosai *"wajazwe maarifa ya mapenzi Yake,"* Wakolosai 1:9.Maombi yako ya dhati kwa ajili yako na wengine yanapaswa kuwa ya kujua na kutekeleza mapenzi ya Mungu.

**Pata mwongozo.** Mungu hufunua mapenzi Yake kwa mtu binafsi kupitia Neno Lake, hekima Yake, watu Wake, na amani Yake. Mwombe Mungu akufunulie mapenzi Yake. Atajibu maombi yako kupitia:

1. Neno Lake. Kujua mapenzi ya Mungu kwako binafsi kunatokana na tabia ya kujifunza Biblia. Mapenzi ya Mungu kwako yanakuwa wazi kadiri unavyopata hekima na ufahamu kutoka kwenye Neno Lake. Kamwe hatakuongoza katika jambo linaloenda kinyume cha Neno Lake.

2. Hekima Yake. Hekima ya Mungu inatokana na utiifu wa kiroho, 1 Wakorintho 2:14-15. *"Msifuatishe tena mfano wa ulimwengu huu, bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu. Ndipo mtaweza kujaribu ili kuthibitisha mapenzi ya Mungu yaliyo mema, yanayopendeza na kamilifu machoni pake,"* Warumi 12:1-2. Mwombe Mungu hekima Yake, *"Kama mtu yeyote miongoni mwenu amepungukiwa na hekima, basi amwombe Mungu... naye atapewa,"* Yakobo 1:5.

3. Watu Wake. Watu wa Mungu ni rasilimali ya kutusaidia kuelewa mapenzi ya Mungu. Wale wanaofundisha kwa usahihi Neno Lake kwa kuzungumza na kuandika wanaweza kusaidia, Wakolosai 1:28. Ni vyema kupata ushauri kutoka kwa Waumini waliokomaa. Kuwa na mshauri zaidi ya moja ni wazo zuri, *"Mipango hushindwa kufanikiwa kwa ajili ya kukosa ushauri, bali kukiwa na washauri wengi hufanikiwa,"* Mithali 15:22. Waumini waliokomaa wanaweza kukosea lakini pia wanaweza kukupa maarifa yenye manufaa ili kukusaidia kubaini mapenzi ya Mungu.

4. Amani Yake. Amani ya Mungu ndio thibitisho la mwisho la mapenzi Yake kwa mtu binafsi, *"Amani ya Kristo na itawale mioyoni mwenu,"* Wakolosai 3:15. *"Nayo amani ya Mungu, inayopita fahamu zote, itailinda mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu,"* Wafilipi 4:7. Amani hii ni hisia ya kina ya usahihi wa uamuzi baada ya maombi, kujifunza Biblia, hekima ya kiroho, na maarifa kutoka kwa washauri waliokomaa kiroho. Tafuta na usubiri amani Yake.

**Chukua hatua.** Unapouliza ikiwa jambo fulani ni mapenzi Yake, jibu huenda likawa "la" kama ilivyokuwa kwa Paulo, 2 Wakorintho 12:7-10. Huenda likawa "subiri." Jibu Lake la "subiri" linaweza likaleta baraka kubwa, Isaya 40:31. Jibu la Mungu likiwa "ndio", tekeleza mapenzi Yake hata kama ni magumu, hayapendwi, au ni ya gharama kubwa. Tunapaswa kufurahia kutekeleza mapenzi Yake kutoka mioyoni mwetu, Zaburi 40:8, Waefeso 6:5-6. Jihadhari na majibu bandia yanayofundishwa kama ni Ukristo. Tii ukiwa na uhakika kwamba unajua mapenzi ya Mungu.

---

*Je, Nawezaje Kujua Mapenzi ya Mungu?* © 2026 imeandikwa na John D. Morris III na kuchapishwa na Acts One Eight. Unaweza kuichapisha, kuinakili, kuichapisha mitandaoni, kuituma kupitia barua pepe, au kuituma kama ujumbe bila kubadilisha maudhui yake huku ukijumuisha kauli hii kikamilifu. Unaweza kujumuisha jina la huduma au kanisa lako au nembo kwenye sehemu ya juu ya ukurasa wa kwanza na uweke taarifa zako za mawasiliano juu ya mstari mzito ulio karibu na sehemu ya chini ya ukurasa wa pili. Mafundisho ya WillofGod316.org yanatokana na Biblia pekee. Yanalenga kuwasaidia Waumini kugundua mapenzi ya Mungu. Unaweza kutuma barua pepe kwa Acts One Eight (katika lugha ya Kiingereza ikiwezekana) ukitumia anwani ifuatayo: Hello@Mail316.org. Huduma za utafsiri zimetolewa na www.ChristianLingua.com. *Je, Nawezaje Kujua Mapenzi ya Mungu?* inapatikana katika lugha arubaini na nane bila malipo kwenye www.WillofGod316.org. Nukuu za Maandiko katika tafsiri hii zimetolewa kutoka kwenye Biblia ya Neno.